OFISI YA RAISI - TAMISEMI
HALMASHAURI YA MJI KASULU

SHULE YA SEKONDARI HWAZI
S.L.P 392,
KASULU
14/12/2020.
simu no.**+255755283890**

Kumb Na. HSS/REG 3248/NST/AD/2021/16

JINA LA MWANAFUNZI.....
S.L.P.....
KASULU.

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI HWAZI WILAYA KASULU MKOA WA KIGOMA MWAKA 2021

1.0 Utangulizi

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha **Kwanza** katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari Hwazi ipo umbali wa km2 (Mbili) Mashariki-Kusini mwa mji wa **KASULU**/Halmashauri ya **MJI WA KASULU**.

Muhula wa masomo utaanza tarehe **11/01/2021** unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **25/01/2021** (ndani ya siku 14) Ukichelewa ndani ya muda huo hautapokelewa tena. Tafadhali zingatia muda huo. **English orientation course itaanza tarehe 12/01/2021** na inatarajika kumalizika tarehe **12/02/2021** karibu sana Hwazi sekondari.

2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia
Sare za shule

Hakikisha mwanao ana sare kamili ya shule ifikapo tarehe **11/01/2021.**

2.1 Wasichana: **Anatakiwa kuwa na:-**

1. Shati mbili(2) rangi nyeupe mikono mifupi
2. Sketi mbili(2) rangi nyekundu damu ya mzee, iliyoshonwa style ya linda box, ndefu mpaka usawa wa jicho la miguuni na Tai rangi ya sketi.
3. Soksi (stocking) rangi nyeupe. Nunua jozi mbili au zaidi.

4. T-shirt rangi ya bluu na Bukuta rangi ya bluu au Tracksuit ya rangi ya bluu kwa ajili ya michezo.
5. Kwa wanafunzi wa kike wa kiislamu wanatakiwa kushona sketi ndefu isiyobana inayofika kwenye jicho la mguu.
6. Kanzu nyeupe ya mikono mirefu yenye urefu unaofika usawa wa magoti na hijabu nyeupe (juba)
7. Viatu vya ngozi rangi nyeusi vyenye soli fupi (kisigino kifupi)
8. Raba kwa ajili ya michezo
9. Sweta rangi ya damu ya mzee

2.2. Wavulana : Anatakiwa kuja na :

a) Shati mbili (2) rangi nyeupe mikono mifupi
b) Suruali mbili (2) rangi nyekundu ya damu ya Mzee, (suruali zenye malinda) na tai rangi ya suruali.
c) Soksi rangi nyeusi.
d) Bukta rangi ya kijani na T- shirt rangi ya kijani au Tracksuit ya kijani kwa ajili ya michezo.
e) Raba kwa ajili ya michezo
f) Sweta rangi ya damu yam zee.

2.3 Vifaa vingine ambavyo ni muhimu kuja navyo:

a) Daftari kubwa zisizopungua kumi(10) Mathematical set moja (1) na kalamu za kutosha za wino na penseli.
b) Uje na nakala ya cheti cha kuzaliwa au Affidavity form iliyojazwa na na kuthibitishwa na Mahakama.
c) **Daftari kubwa tatu (3) kwa ajili ya English orientation course ambazo anatakiwa kuripoti nazo tarehe 11/01/2021**.

3. Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na Kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995, Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, yenye dhamana ya elimu chini ya **Ofisi ya RAISI- TAMISEMI** yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

3.1 Mambo ya msingi hayo ni:-

a) Heshima kwa viongozi, wazazi,wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

g) Kuvaa sare ya shule wakati wote, na
h) Kutunza mali za umma.
i) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

3.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule:-

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji.
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
e) Kupigana au kupiga.
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
g) Kudharau Bendera ya Taifa.
h) Kuwa mjamzito/Kupata mimba.
i) Kuoa au kuolewa
j) Kutoa mimba
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
l) Kukataa adhabu kwa makusudi
m) Kuwa na simu ya mkononi.

4.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.

a) Medical Examination form, ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.
b) Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshirirki, katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatayotolewa na shule.
d) Nakala ya cheti cha kuzaliwa au Affidavity form

5.0 Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

.....

JONATHAN TIMOTHY
MKUU WA SHULE

THE HEADMASTER
HWAZI SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 392, KASULU.

HALMASHAURI YA MJI KASULU

SHULE YA SEKONDARI HWAZI
S.L.P.392,
KASULU.

SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

A. MSIMAMO WA SHULE.

1. Nidhamu ya hali ya juu nyakati zote – Exemplary Discipline
2. Taaluma kiwango cha juu – Academic Excellence
3. Usafi wa hali ya juu – High standard of smartness
4. Lugha ya mawasiliano ni Kiingereza.

B. SHERIA ZA SHULE.

Makosa yafuatayo ni makubwa. Mwanafunzi anayepatikana na makosa haya anafukuzwa shule moja kwa moja.

i. Wizi wa aina yoyote pamoja na kumiliki simu ya aina yoyote.

ii. Udanganyifu katika mitihani ya aina yoyote.

iii. Kujaribu, kusababisha au kuongeza na kushiriki kugoma kwa wanafunzi.

iv. Uasherati

v. Ulevi wa aina yoyote pamoja na tuhuma za kunywa pombe.

vi. Uvutaji sigara, bangi, madawa ya kulevya, ugoro, kubeli au kujichubua mwili kwa vipodozi (skin creams/ lotions).

vii. Makosa ya jinai na kusimamia au kuongeza itikadi za kidini.

viii. Ugomvi, lugha chafu, kupigana na kugoma adhabu.

ix. Kuharibu mali ya shule hasa madawati na viti anavyovitumia.

x. Kuolewa au kuoa na tuhuma za mapenzi na wanafunzi wenzake au nje ya wanafunzi wenzake.

xi. Kupata mimba au kusababisha mimba.

xii. Kupatikana na kosa la kutoongea lugha ya Kiingereza mara kwa mara.